

KUTENGENEZA KALENDA YA KIISLAMU YA MAWIMBI YA BAHARI (THE ISLAMIC TIDES CALENDAR)

Kutoka Dar es salaam LAT 6°50'S, LONG 39°17'E mpaka Zanzibar LAT 6° 10'S – LONG 39° 11E pana tofauti ndogo ya masafa juu ya duara la dunia.Pia kuna tofauti ndogo za muda wa maji kupwa na maji kujaa.Zaidi ya hivyo, tofauti zote hizi ni ndogo sana kuweza kuzingatiwa kama tofauti za kuathiri nyongeza ya muda mawimbi makuu yanaposogea katika muda wa siku nzima.Hivyo hata ukichukua maeneo ya mbali zaidi yenye tofauti kubwa za longitude,ambao ndio usawa wa mizunguko ya mwezi na mawimbi juu ya dunia,bado tofauti haibadili tarehe ya siku husika.

Ili kupata kalenda ya mfano ya kiislamu ya mawimbi ya bahari,tutatumia kalenda nne tofauti za kiislamu kama zilivyochapishwa mwaka 2006.Mbili kati ya hizo kwa mtazamo wangu zina msimamo wa mwezi wa kimataifa na mbili ni za msimamo wa kila nchi na mwezi wao.Kalenda tunayotarajia kuitayarisha itakuwa ni tofauti na kalenda zote hizo tulizozitaja.

Tumeona kuwa kwa mujibu wa Qur'an (10:5) mizunguko ya Jua,Mwezi,dunia na sayari zote kwa ujumla ni kwa mahesabu maalum ambayo Mwenyezi Mungu amevikadiria. Hivyo muda ambao mwezi hukamilisha mzunguko wake kuizunguka dunia utakuwa ni muda muhimu tutakaoutumia kujua mwanzo wa siku na mwezi mpya.

Kulingana na maelezo kwenye mjadala uliotangulia (Mawimbi kama kioo..) siku yetu na mwezi mpya vitaanza alfajiri ya mwanzo baada ya mwezi kukamilisha mzunguko wake wa kuizunguka dunia.

Kabla ya kujadili namna ya kutengeneza kalenda ya kiislamu ya mawimbi ya bahari mwezi baada ya mwezi,hapana budi kuelewa misamiati mitatu ya kalenda hii,nayo kwa ufupi ni SFT au sft,SMT au smt na NMS au nms kama ilivyo hapo chini.

ALFAJIRI YA KWELI (SFT,sft)

Mawimbi makuu ndiyo yanayotumika kuiongoza siku na kuitolea taarifa.

Watakaoiongoza siku na wakawa wa mwanzo kutekeleza ibada kama ya funga ya Ramadhani,ni wale watakaofikiwa na wimbi kuu mburuziko si chini ya nusu saa kabla ya alfajiri ya kweli-Standard Fajr Time(SFT) na baada ya mwezi kuanza mzunguko mpya.

Mawimbi makuu kama tulivyoona katika mada nyengine zilizotangulia katika mjadala huu,mojawapo ni lazima litakuwa limefika eneo fulani la dunia katika muda usiofikia masaa 7.

Ili siku ya kiislamu iwe moja na isiyowababaisha waislamu,basi wimbi kuu litakalotumika kuamua mwanzo wa siku ni lile la mburuziko pekee hata ikiwa kulisubiri kwake ni kwa masaa 12 ambako ni kabla ya siku moja yenye masaa 24 kumalizika.

Ili kujua kuweka muda maalum wa alfajiri ya kweli nimechukua nyakati zote za sala ya alfajiri kwa mwaka mzima katika ratiba ya swala kwa saa za zoni iliyotengenezwa na marehemu sheikh Abdullah Saleh Farsy.Hizi zitakuwa ni nyakati kwa kufuata mwendo na mwangaza wa Jua.Kwa upande mwingine nikajumlisha nyakati zote za mawimbi makuu kwa kila mwezi mwandamo baada ya mwezi kuanza safari yake ya mzunguko mpya.

Nyakati zote za mawimbi makuu kwa pamoja nikajumlisha na nyakati zote za swala ya alfajiri na kutafuta wastani wake.Matokeo yakawa ni saa 10.59 ambayo kwa ukaribu nimeiita ni saa 11.0 alfajiri..Muda huu ndio ninaopendekeza kuitwa alfajiri ya kweli

(sft),Baada ya takriban miaka miwili tangu kufanya jumla hizo nimekutana na ratiba ya swala kwa mji wa Mombasa iliyotolewa na Dkt Khalid Shaukat, ambaye kwa ujumla atakuwa ametumia utaalamu zaidi wa elimu ya anga aliyonayo, Kwa haraka nimeiona haina tofauti sana na ile ya sheikh Abdullah Saleh Farsy, hivyo bado alfajiri ya kweli itabaki ni muda huo huo wa saa 11.0 alfajiri.

MAGHARIBI ILIYOTIMIA (SMT, smt)

Kwa vigezo kama hivyo tunahitaji kuwa na magharibi iliyotimia kinyume cha alfajiri ya kweli. Magharibi hii tutaita Standard Magharib Time (SMT). Kwa mwaka 2006 kila mwezi tumechagua siku tatu, tarehe 1, 11 na 21. Tukijumlisha nyakati zote za kuzama kwa jua (sunset) kwa mji wa Tanga tunapata wastani wa saa 1826.67. Kwa ukaribu wa takwimu tunachukulia ni saa 1830 ambayo ni saa 12.30 magharibi. Huu ni muda ambao kwa maeneo ya Afrika Mashariki huwa ni tayari kwa ibada ya swala ya magharibi na kufuturu kwa ibada ya funga.

Kwa vile tofauti za mawimbi makuu kwa maeneo yaliyo karibu ni ndogo sana, tunaweza kujadili kituo chochote kati ya Zanzibar, Dar es salaam, Tanga au Mombasa na jawabu itakayopatikana ikatosheleza kwa eneo jengine kati ya haya na kuwa vigezo kwa maeneo mengine ya mbali..

NEAR MAGHRIB SIDE (NMS, nms)

Ni sehemu maalumu au mjumuiiko wa masafa karibu na mstari wa longitude ya upande wowote wa dunia kulingana na mtu alipo, ambapo wakati mwezi unaanza safari mpya ya kuizunguka dunia basi eneo hilo kwao itakuwa ni magharibi.

Magharibi kikawaida ni muda ambao mwezi huchomoza na kuonekana kwa mara ya mwanzo pindi hali ya hewa ikiruhusu. Eneo hili hujulikana kwa kupata wimbi kuu mburuziko (wkmb).

Mwezi Muharram 1427-H ulianza saa 1715 (saa 11.15 jioni) kituo cha Dar es salaam. Hii ni baada ya kukamilisha mzunguko wake uliotangulia. Muda huu ndio unaoitwa wa kuanza *new moon* na ni muda ambao mwezi hauonekani popote duniani kwa macho, lakini hujitokeza kwa uwazi zaidi kupitia mawimbi ya bahari.

Near maghrib side (nms) iko mashariki ya Dar es salaam.

Kufikia SMT ni tofauti ya saa 1.15. Hizi ni jumla ya dakika 75. Ikiwa dakika nne ndio muda inaochukua kukatiza longitude 1. Hivyo dakika 75 itakuwa ni $(75/4)^0 \text{ long} = 18.75^0 \text{ long}$ mashariki ya Dar es salaam. Kwa vile Dar es salaam penyewe ni longitude 39 ukijumlisha na 19 unapata longitude ya 58.

Kwa mashariki ya Dar es salaam 58^0 inaangukia katikati ya bahari ya hindi maeneo yasiyokaliwa na watu. Kwa kaskazini, longitudo hii inapitia nchi za Iran, Turkmenistan, Kazakhstan na kadhalika. Maeneo yanayopitiwa na longitude hii ndiyo ambayo kwa wastani watakuwa wako muda wa magharibi wakati mwezi ukianza mzunguko mpya.

Mwezi unapoanza mzunguko wake mpya daima unakuwa uko karibu sana na *ecliptical plane*, yenye maana kuwa nguvu ya kuyavuta maji ya bahari ni kubwa zaidi. Hivyo kwa kujua maeneo ambayo mwezi unapoanza mzunguko huu mpya kwao ni magharibi (SMT) inakuwa ndio tumejua eneo la wimbi kuu mburuziko (WKMB).

Hii ina maana kuwa kwa mwezi muharram 1427-H maeneo ya longitude 58° ndiyo yaliyoanza kupata wimbi kuu mburuziko na ndio mwenyeji kwa ugeni wa mwezi huo. Siku kwa wenyeji hawa ingeanza alfajiri inayofuata ambayo kufikia saa 11 alfajiri ni masaa 10.30 mbele.

Siku ingeanza muda huo, na kama ni ibada ya funga utapatikana muda wa kutosha kwa matayarisho yake mfano kwa ajili ya daku. Waislamu wengine wote duniani wangetakiwa kuwa nyuma ya watu wa maeneo haya ya 58° long, kama ilivyo kwa Dar es salaam hata kama kwa teknolojia iliyopo watapata taarifa hii mapema.

Kama tulivyoona kabla kuwa, kwa muda wa masaa 24 mawimbi makuu husogea kidogo tu kwa wastani wa saa 1. Hivyo wenyeji wa mwezi Muharram wangeondoka na kusogea mbele juu ya dunia, lakini wimbi kuu lingebaki na kusogea kidogo kutoka hapo kwa masaa 24 yajayo. Wote ambao wako nyuma (magharibi ya 58°) wangelipitia wimbi hili. Hivyo hivyo kwa wimbi kuu mmiminiko (WKMM).

Wimbi kuu ambalo kila mmoja atakutana nalo wakati wa alfajiri ni lile la mmiminiko ambalo katika muda wa masaa 12 tangu wakati wa SMT huwa limesogea kidogo zaidi katika muda huo.

Kwa upande wa tarehe kwa kalenda ya kizungu, saa 1715 sawa na 11.15 kwa saa za Afrika Mashariki mwezi ulipoanza mzunguko wake mpya ilikuwa ni tarehe 29 Januari 2006. Alfajiri iliyofuatia ilikuwa iko tarehe 30 Januari. Kwa vile siku ya kiislamu inamalizikia tena alfajiri baada ya masaa 24, alfajiri ambapo ingemalizikia na kuanza siku nyengine ingekuwa ni Januari 31, 2006.

Iwapo ni lazima tarehe zetu zitajwe na tarehe hizi za kizungu, hivyo mwezi mosi Muharram uliingia kwenye tarehe hizo, mbili, nazo ni Januari 30 na 31 kwa kigezo cha wenyeji.

Itakuwa ni jambo la kushangaza waislamu kushutumiana kwamba mwezi uliandama tarehe 30 Januari, mbona wengine walianza kufunga tarehe 31 Januari!, Kwetu waislamu hiyo bado ilikuwa ni siku moja tu.

Ukiangalia mwenendo wa mawimbi ya bahari kwa kituo cha Dar-es-salaam. Alfajiri ya tarehe 30 Januari kulikuwa na wimbi kuu mmiminiko (wkmm) la 3.82m nyakati za 0435hr. Wimbi la maji kupwa lililofuata ni 0.07m nyakati za 1056hr. Tofauti baina yao ni $3.82m - 0.07m = 3.75m$

Alfajiri ya tarehe 31 Januari kulikuwa na wimbi la maji kujaa la 3.89m nyakati za 0514hr na kufuatiwa na wimbi la maji kupwa la -0.33m nyakati za 1130hr. Tofauti baina yao ni $3.89m + 0.33m = 4.22m$

Funga kwa Dar es salaam (Tanzania), ilianza alfajiri tarehe 30 Januari na wimbi kuu mmiminiko (wkmm). Ni masaa takriban 12 tangu mzunguko mpya wa mwezi kuanza. Jioni yake mwezi ungeweza kuonekana katika baadhi ya maeneo ya Tanzania. Kumbukumbu za mtandao wa moonsighting.com zinaonesha kuwa Hamza Rijali wa Zanzibar aliuona mwezi siku hiyo na kwamba mufti wa Zanzibar alitangaza kuanza kwa funga tarehe 31 Januari 2006.

.....

...

Nms E, day at immediate fajr, range second large

Mwezi Safar -1427H: Ulianza safari tarehe 28 Februari 2006 saa 0331 kituo cha Dar-es-salaam. Hii ni sawa na saa 9.31 karibu na alfajiri.

Near maghrib side (Nms) ni upande wa magharibi kutokea Dar-es-salaam. Hili ni eneo ambalo kwao ndio kwanza magharibi inaingia wakati ambapo kwa Dar es salaam ndio kunakaribia kucha.

Kwa vile SMT ni saa 12.30, hivyo kutokea Dar-es –salaam ambako ni saa 9.31 karibu ya alfajiri, kutakuwa na tofauti ya masaa 10.1 sawa na dakika 601. Hii ni sawa na $(601/4)^0$ longitude, ambazo ni $150^0 15'$ magharibi ya Dar es salaam.

Tunarudi nyuma 39^0 kwanza mpaka 0^0 greenwich meridian, halafu $111^0 15'W$ ($39+111.15=150.15$).

Ukiangalia kwenye ramani kwa usawa wa equator, eneo hili linaangukia katikati ya bahari ya pacific, maeneo yasiyokaliwa na watu. Kwa kaskazini, longitude ya $111^0 W$ inapita mashariki ya nchi ya Mexico kwa kaskazini, eneo la Hermosilo. Vile vile inapita katikati ya America maeneo kama vile Montana na pia Canada karibu na Edmonton.

Maeneo hayo ndiyo wenyeji wa mwezi wa Safar 1427 H. Siku ingeanza wakati itakapoingia alfajiri kwao. Wengine wote hata wakipata taarifa juu ya kuonekana mwezi wangesubiri mpaka maeneo hayo yaianze siku ya kiislamu na matendo ya kiibada yanayoambatana na siku hiyo.

Kwa kalenda ya kizungu, tarehe 28Feb Dar –es –salaam ilikuwa mbele ya long $111W$. Hivyo Hermosilo; Mexico na maeneo yaliyotajwa hapo juu ilikuwa ni saa 12.30 jioni tarehe 27Feb; 2006. Masaa 10 baadae ndipo wangeingia alfajiri ambayo ni tarehe 28Feb, huku Dar es salaam ikiwa ni saa 7.30 adhuhuri tarehe hiyo.

Siku hiyo ya kiislamu, watu wa Dar es salaam (Tanzania) wangepanua kukutana nayo alfajiri ya tarehe 01 March na wangepimaliza alfajiri ya tarehe 2 March. Wangepanza tena kama Muharram kwa wimbi kuu mmiminiko (wkmm).

Watu wa America na Canada ambao walikuwa mbele kwa tarehe ya kiislamu, wangepanza siku hiyo tarehe 28 Februari na kuimaliza tarehe 01 March. Hivyo wao ndio wenyeji na dereva wa siku kwa tarehe ya kiislamu kwa mwezi huo. Wote wengine wangepanua nyuma yao.

Kwa ulinganisho na kalenda hiyo ya kizungu (kikristo) hatukuwa na sababu ya kushangaa kwamba wako waliouanza mwezi Safar tarehe tofauti za March na Februari.

Tuangualie hali za mawimbi mnamo tarehe 01 March 2006 kituo cha Dar-es-salaam, siku ya mwezi 1 Safar. Muda wa saa 0459hr (saa 10:59 alfajiri) kulikuwa na wimbi kuu la ukubwa wa 3.93m. Masaa 6 baadae maji yalikutwa mpaka -0.12m. Tofauti kati ya mawimbi haya ya maji kupwa na maji kujaa ni $3.93+0.12 = 4.05m$, ndiyo tofauti kubwa kwa mwezi huo.

Kumbukumbu za kuonekana mwezi kutoka moonsighting.com inaonesha baadhi ya maeneo waliouona mwezi tarehe 28 ni pamoja na Ghardaia (Algeria), Roseau (Dominica), Richmond (Virginia-US), Houston (US) na maeneo mengine ya Amerika. <http://www.moonsighting.com/1427sfr.html>

Hamza Rijal (MCW) kutoka Zanzibar katika moonsighting ameripoti kutokuuona mwezi kwa macho tarehe 28 na hakukuwa na habari za sehemu nyengine za visiwa hivyo kuonekana, hivyo akasema tarehe rasmi ya mwezi 1 Safar ingekuwa tarehe 2 March 2006. Hiyo ni takriban masaa 48 tangu mwezi ulipoanza kujitokeza na kuanza safari zake kwa mwezi huo. Kulikuwa na wimbi la 3.88m saa 0534 liliofuatiwa na -0.13m saa 1140. Tofauti baina yao ni 4.01m.

.....

Nms W,day begins late,range largest

RABIUL AWWAL 1427: Ulianza safari mpya saa 1315 sawa na saa 7.15 aduhuri kituo cha Dar-es-salaam tarehe 29 Machi 2006 .Near maghrib side (nms) ni mashariki ya Dar-es –salaam.

Kufikia SMT (ya nyakati za am na pm) ni masaa 5 na robo ; $7.15+5.15=12.30$
Masaa 5.15 ni sawa na dakika 315 ambayo ni sawa na $315/4$ longitudes= 79° long.E ya Dar es salaam.Tunakwenda nyuzi 79 mashariki ya Dar-es –salaam.Kutoka 39° E tunafika 118° E($39+79$).Eneo hili ni katikati ya Indonesia kwenye visiwa vya Sunda kwa usawa wa ikweta.Kusini inapita magharibi ya Australia.Kwa kaskazini inapita nchi za Malaysia,Philipines na mashariki ya China.

Hivyo Indonesia na maeneo ya nchi tulizozitaja ndiyo wenyeji na waongozaji wa mwezi Rabiul awwal 1427H.Siku ingeanza kwao itakapoingia alfajiri na wengine wote hata wakipata taarifa juu ya kuanza huku kwa siku wangepaswa wafuatie nyuma ya maeneo hayo.Siku hiyo ni tarehe 30 Machi kwa nyakati za kalenda ya wakristo.Alfajiri ambayo siku hii ingemaliza kupisha siku nyengine ingekuwa ni tarehe 31 Machi 2006.

Kutokana na upana wa nchi ya Indonesia na mabadiliko ya nyakati,ingewezekana kwa baadhi ya maeneo kutoweza kuianza siku ya kiislamu siku hiyo na kuianza tarehe 31March .Haya ni kila eneo humo ambalo kabla kufikia alfajiri ya kweli (SFT), tofauti ya muda ni chini ya nusu saa,na hasa kwamba muda unaoruhusika kula daku umepita kwao.

Tanzania kwa kigezo cha Dar es salaam siku ya mwanzo ya mwezi Safar ingekuwa ni tarehe hiyo hiyo 30Machi 2006.Inapofika wakati wa SFT kwa Dar es salaam watu wa maeneo ya NMS hasa visiwa vya Sunda ;Indonesia wangukuwa kwao ni saa 4.15 asubuhi kwa nyakati za kalenda ya kikristo.

Jioni ya tarehe 29 saa 1624hr kulikuwa na wimbi la 3.89m lililofuatiwa na wimbi la maji kupwa la 0.09m saa 2228hr.tofauti ni $3.89m-0.09m=3.8m$.Alfajiri ya Machi 30 kulikuwa na wimbi kuu la 3.81m nyakati za 0438hrs,ikafuatiwa na wimbi la maji kupwa la -0.05m saa 1041hrs.Tofauti baina yao ni $(3.81+0.05)m=3.86m$.Wimbi la 3.89m ni WKMB na 3.81m ni WKMM.Baadae kukawa na wimbi la 4.05m muda wa 1657hrs lililofuatiwa na wimbi la maji kupwa la 0.03 muda wa 2304hrs.Tofauti baina yao ni $(4.05m-0.03)=4.02m$.Tarehe 31 muda wa 1733hrs kulikuwa na wimbi la 4.08m lililofuatiwa na 0.10m muda wa 2341hrs ,tofauti baina yao ni 3.98m.Hii ni zaidi ya 48hrs tangu mwezi uanze safari yake ya mwezi Safar.

Kumbukumbu za kuonekana mwezi zinaonesha maeneo yaliyoweza kuuona mwezi kwa urahisi ni Zanzibar mara baada ya magharibi saa 1840 tarehe 30Machi 2006 kama ilivyoripotiwa na Hamza Rijal wa moonsighting.com(<http://www.moonsighting.com/1427rba.html>).

Maeneo mengine waliouona ni Lilongwe(Malawi),Oslo(Norway) pamoja na maeneo mengi ya nchi ya Amerika na Canada.Kwa vigezo hivi siku ya mwanzo kwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla ingekuwa tarehe 31Machi, ambayo kwa vigezo vyetu ingekuwa ni mwezi 2Rabiul awwal.

.....
Nms E,day begins immediate fajr, largest range (4.02m) with in 24hrs.

RABIU THANI 1427H: Ulianza safari yake muda wa 2244hrs sawa na saa tano kasoro dakika 16 (10:44pm) usiku tarehe 27April 2006 kituo cha Dar es salaam.

Near maghrib side (nms) ni magharibi ya Dar -es-salaam.Kwa vile Standard maghrib time (SMT) ni saa 12.30 magharibi,hivyo tofauti ya muda wa mwezi kuanza safari na SMT ni wastani wa masaa 4 na robo,sawa na dakika $\{(60 \times 4) + 15\}$ =dakika 255.

Dakika 255 ni sawa na nyuzi $255/4 = 63.75$ long au wastani wa nyuzi 64 magharibi ya Dar es salaam.Kutoka Dar es salaam $39^{\circ}E$ tunarudi nyuma 64° ambayo ni $64-39=25$ kufikia Greenwich.Halafu tunakwenda $25^{\circ}W$ (magharibi ya Greenwich). Kwenye ramani ya dunia eneo hilo linaangukia katikati ya bahari ya pacific,maeneo yasiyokaliwa na watu kwa pande zote za ikweta,kaskazini na kusini.Nchi za karibu zenye kukaliwa na watu ni zile za magharibi ya Afrika kama vile Senegal,Mauritania na Morocco.

Nchi hizo za magharibi ya Afrika tutazibebesha uwenyeji na uongozi wa mwezi wa Rabiul thani 1427H.Siku ingeanza itakapoingia alfajiri kwao ambayo kwa kalenda ya kizungu(kikristo) ingekuwa ni tarehe 28April 2006 na ingemalizikia tarehe 29April2006.

Katika nchi za maeneo hayo kila ambaye angekuwa na muda wa kutekeleza ibada ya swala au ya funga kabla ya kupita SFT angekuwa ameipata siku ya mwanzo ya Rabiul thani na zaidi hapo siku ingekuwa imemponyoka na angesubiri kesho yake.Kwa hivyo suala la kuwa tofauti ya siku katika eneo fulani haliepukiki,hata hivyo ni kwa vigezo maalum na siku ingebaki ni moja tu.

Uzuri wa tofauti hii ya siku ni kuwa kinyume na ilivyo sasa haitokuwa ni jambo la kubahatisha na itajulikana kabla kwa vigezo maalum,hivyo hakutokuwa na mzozo wa kikalenda kwa waislamu.Kwa vile alfajiri kwa waislamu haiko mpakani mwa siku ya kizungu tarehe 28/29 April itakuwa si za kujadiliwa tena.

Kwa maelezo hayo mwezi mosi Rabiul thani kwa Dar-es-salaam na Tanzania yote ilikuwa ni tarehe 29April,kwani kwa kalenda ya kikristo Tanzania iko mbele ya nchi za Afrika magharibi lakini kwa kalenda ya kiislamu ilipaswa iwe nyuma ya nchi hizo.Tarehe 28 nyakati za alfajiri (sft) Dar es salaam ilikuwa tayari ni saa 3.15 asubuhi.Hii ilikuwa ni siku bora kwa Tanzania kuuona mwezi kwa macho jioni yake bila shida yoyote kwani tangu uanze safari yake ni zaidi ya masaa 17 ambapo mwezi tayari huwa umetoka eneo la kufifia nuru yake kutokana na ukali wa mwangaza wa Jua.

Tukija kwa upande wa mawimbi ya bahari.Nchi za magharibi ya Afrika ndizo ambazo zilikutana na wimbi kuu mburuziko (wkmb) nyakati za magharibi,wimbi kuu mmiminiko (wkmm) lilikuwa lipo alfajiri ya kwao;tofauti ya wastani wa masaa 12.Eneo hili ni wastani wa $165^{\circ}E$.Hili pia ni eneo ambalo kwa kiasi kikubwa halikaliwi na watu.Eneo la karibu ni visiwa vya Marshals (Marshal islands).

Tanzania tulikutana na wkmm mara ya mwanzo tarehe 28 saa 10.52 alfajiri(0452hr) likiwa na ukubwa wa 3.52m.Ilipofika jioni saa 10.34 (1634hr) tulikutana na wimbi kuu mburuziko (wkmb) likiwa limepungua mpaka 3.95m hata hivyo ndilo wimbi kuu pekee kwa mwezi huo lililoambatana na muda wa kuungalia mwezi kwa macho.Wimbi la maji mauka dogo zaidi kwa mwezi huo ni 0.14m saa 4.45 usiku lililolifuatia wkmb.Tofauti baina yao ni $3.95m-0.14m=3.81m$ ambayo ndiyo kubwa zaidi.

Mwezi mosi rabiul thani yenyewe kulikuwa na wimbi la 3.46m saa 10.52 alfajiri (0452hr) ambalo ndilo wkmm likiwa linazidi kupungua.

Kumbukumbu za kuonekana kwa mwezi kutoka moonsighting.com (<http://www.moonsighting.com/1427rbt.html>) zinaonesha kuwa hakuna taarifa za kuonekana kwa mwezi tarehe 27 na kuwa tarehe 28 ndio mwezi mosi wa Rabiul thani.Mwezi mosi kwa baadhi ya maeneo ilikuwa tarehe 29 na mengine ilikuwa tarehe

30April.Maeneo yaliyoripotiwa kuuona mwezi tarehe 28 ni ya nchini Marekani tu kama vile South Carolina,Arizona na Washington.

Kwa mfumo wa kuangalia mwezi kwa macho hiyo ni sahihi,hata hivyo siku kwa kufuata mtazamo kwa mawimbi ya bahari ilipaswa kuanza tarehe hiyo 28 kwa kufuata wenyeji waliokuwa NMS.

.....
NMS ni W,day begins later fajr,largest range with in 24hr in first day (28april) of the host.

JAMAADUL AWWAL 1427H:

Mwezi ulianza safari yake muda wa (0826hr) sawa na saa 2.26 asubuhi tarehe 27 May 2006.Nms iko mashariki ya Dar es salaam.Kwa vile SMT ni saa 12.30 magharibi,hivyo tofauti ya muda tangu kuchomoza mwezi ni wastani wa masaa 10.

Masaa 10= dakika $60 \times 10 = 600$.Hii ni sawa na $600/4 \text{ long} = 150^0 \text{ long}$.
Kutokea Dar es salaam (39^0E) tunakwenda nyuzi 150 na tutafika 171^0W .Kwenye ramani ya dunia kwa usawa wa ikweta eneo hili linaangukia katikati ya bahari ya pacific.Ni maeneo yasiyokaliwa na watu kusini na kaskazini.Maeneo ya karibu yanayokaliwa na watu ni visiwa vya Kiribati karibu na ikweta na magharibi kidogo ya 171^0W .Kwa kusini maeneo ya karibu na kwa magharibi ya 171^0W ni visiwa vya Fiji na New Zealand.

New Zealand,Fiji na Kiribati ndio wenyeji (host) mwezi Jamadul uwlaa 1427H kwa muda wote ambao wangeipata SFT.Wote waliobaki maeneo hayo na kote duniani wangepaswa wafuatie nyuma ya wakazi wa maeneo haya hata kama ingejulikana kutokana na teknolojia iliyopo kuwa mwezi umeonekana kwa namna yoyote ile, au siku ingeanza na watu wa maeneo hayo.

Siku yenyewe ingeanza inapoingia alfajiri (sft) kwa wakazi wa Kiribati na jirani zake.Kwa kalenda ya kikristo alfajiri ambayo ingefuatia Kwa Kiribati ilikuwa ni tarehe 28May 2006,ingeishia alfajiri inayofuatia ambayo ni masaa 24 baadae.Hii ingekuwa ni tarehe 29May.Hivyo mwezi mosi Jamaadul uwlaa ulikuwa baina ya tarehe 28-29May 2006.Kwa Tanzania kigezo cha Dar es salaam,mwezi mosi Jamaadul uwlaa 1427H ilikuwa ni kuanzia alfajiri tarehe 28May 2006.

Jioni ya tarehe 27May kituo cha Dar es salaam kulikuwa na wimbi kuu la ukubwa wa 3.70m muda wa saa 10.14.Wimbi hili ni wkmb na ndilo kubwa pekee kwa mwezi huo,ni lile lililopatikana maeneo ya Kiribati ambalo watu wa maeneo hayo waliliwacha hapo.Lilifuatiwa na wimbi la maji kupwa la ukubwa wa 0.32m muda wa 4.32 usiku.Hili nalo ndilo dogo zaidi kwa mwezi huo.Tofauti baina yao ni $(3.70-0.32)=3.38\text{m}$ na ndiyo kubwa zaidi.

Alfajiri ya tarehe 28 mnamo saa 10.39 kulikuwa na wimbi kuu la ukubwa wa 3.14m.Hili ni wkmm,lililofuatia ni la maji kupwa la ukubwa wa 0.50m saa 4.29 asubuhi.

Kumbukumbu za kuonekana mwezi za moonsighting.com (<http://www.moonsighting.com/1427jmo.html>) zinaonesha kuwa yapo maeneo mengi ya Marekani ambao waliweza kuuona mwezi jioni ya tarehe 27 May.Hamza Rijal na Yussuf Lambert wa Zanzibar waliripoti kuuona mwezi kwa urahisi jioni ya tarehe 28 May.

.....
Nms iko E,day next Fajr,Highest range with in 24hrs since new moon.

JAMAADU THANI 1427 H

Mwezi ulianza safari yake muda wa saa 1905hrs sawa na saa 1:05 magharibi kituo cha Dar es salaam mnamo tarehe 25 Juni 2006.

Nms iko magharibi ya Dar-es salaam.Tofauti ya muda ili kulifikia eneo hilo ni (1905-1830)hrs=35min.Hii ni sawa na nyuzi za longitude $35/4 = 8.75$ ambayo ni wastani wa 9^0 long.

Ukiangalia kwenye ramani maeneo ambayo ni 9^0 long magharibi ya Dar-es salaam (30^0 longE) ni Uganda kwa usawa wa Ikweta.Kaskazini ni Sudan,Misri na nchi kadhaa za Ulaya.Kwa kusini ni Rwanda,Burundi,Congo.Inateremka chini zaidi kupitia Congo,Zambia,Zimbabwe mpaka Afrika Kusini (SA).

Hivyo nchi hizi Tanzania ikiwemo ndio wenyeji wa mwezi wa Jamadul Thani 1427H.Siku ingeanza inapoingia sft,alfajiri inayofuatia.Kwa kalenda ya kikristo ni tarehe 26 Juni 2006.Ingedumu mpaka alfajir inayofuatia ya tarehe 27Juni 2006.Waislamu wengine wote duniani hata kama wangepata taarifa mapema basi walitakiwa wafuate nyuma ya nchi hizi katika kuinza siku ya mwezi mosi ya Jamadu thani 1427H.

Takwimu za mawimbi ya bahari zinaonesha jioni ya tarehe 25 kulikuwa na wimbi kuu la ukubwa wa 3.45m saa kumi na dakika nne (1604hrs),lililofuatiwa na wimbi la maji kupwa la 0.46m saa 4.26 usiku.Alfajiri ya tarehe 26 mnamo saa 10.38 kulikuwa na wimbi kuu la ukubwa wa 2.93m.

Wimbi kubwa zaidi katika mwezi huu ni lile la jioni saa kumi na moja kasorobo (1645hr) la ukubwa wa 3.46m tarehe 26Juni lililofuatiwa na wimbi dogo zaidi la maji kupwa la ukubwa wa 0.44m saa 5.04 usiku (2304hr).Wimbi la 2.93m ni wkmm na hili la 3.46m ni wkmb lililofanyika mnamo smt ya tarehe 25Juni,ambalo tunakutana nalo tena jioni hiyo ya tarehe 26Juni.

Kabla kuangalia kumbukumbu za kuonekana mwezi na uanzaji wa mwezi huu wa Jamadul Thani 1427,tunakisia kwamba huu ni mmoja ya miezi iliyokuwa na mzozo baina ya waislamu.Ni mmoja wa mwezi ambao tofauti baina waislamu wa maeneo haya yangetokea na kukubalika kwa vile wenyeji wa mwezi huu ni wao.Kwa vigezo vyetu wangepatikana watu ambao wangeikosa sft.

Tukiangalia kumbukumbu hizo za kuonekana mwezi kutoka <http://www.moonsighting.com/1427jmt.html> tunaona kuwa hakuna nchi iliyouna mwezi tarehe 25.Kufuatana na kumbukumbu hizo mwezi ungeweza kuonekana kirahsi tarehe 26 kwa ujumla maeneo yote yaliyo magharibi ya Nms tuliyoitaja humu,lakini kwa taarifa ya Hamza Rijal hata tarehe 26 hakuweza kuuona mwezi maeneo ya Zanzibar.

Maeneo yaliyoweza kuuona mwezi kwa macho tarehe 26 Juni ni Berlin nchini Ujerumani na baadhi ya maeneo ya Marekani tu.Kwa hali hiyo waislamu walio wengi duniani walianza kuhesabu mwezi mosi Jamaadul thani kuanzia tarehe 28Juni 2006, takriban siku 3 tangu mwezi uanze mzunguko wake mpya.

.....
Nms W,immediate next sft.Wkmb with in 24hrs,Range btwn high and low tides the highest.

MWEZI RAJAB 1427 H

_Mwezi ulianza safari yake muda wa saa 0731hrs sawa na saa 1:31 asubuhi kulingana na kituo cha Dar –es –salaam mnamo tarehe 25Julai 2006.

Upande wa dunia ambao muda huo kwao ni magharibi ni mashariki(+) ya Dar-es salaam. Tafauti ya muda kufikia smt ni masaa 11 ambao ni sawa na nyuzi za longitudo $660/4=165^0$ long.

Kutokea Dar es salaam (39^0E) mpaka International date line itakuwa tumekwenda nyuzi 141.Nyuzi 24 zilizobakia ndani ya upande wa magharibi wa Greenwich zitatupeleka mpaka 156^0 long W;(180⁰W-24⁰).

Mstari huo wa longitude kwa karibu na ikweta miongoni mwa maeneo yanayokaliwa na watu unapita visiwa vya Kiribati.Kwa kaskazini unapita jimbo la Alaska la Marekani. Hivyo maeneo hayo ndio wenyeji kwa mwezi Rajab 1427H.Wengine wote watakuwa wako nyuma ya wakazi wa maeneo haya.

Kulingana na mapitio ya mstari wa international date line Kiribati iko tarehe tofauti kuliko ilivyopaswa kwa mtazamo wa kalenda ya kikristo iliyozeleka.Kwa upande wetu hali hiyo haitozingatiwa.Hata hivyo kwa matumizi ya kalenda yetu ya kiislamu hali hiyo itakubalika kwa vile maeneo yote yanayokaribiana na Kiribati hayakaliwi na watu.

Siku ingeanza wakati wa alfajiri inayofuatia kwa wakazi wa Kiribati.Hiyo ingekuwa ni tarehe 26Julai 2006.Siku ingedumu kwa masaa 24 mpaka alfajiri ya tarehe 27Julai.

Kwa Dar es salaam siku ingeanza tarehe hiyo 26 takriban masaa 11 tangu Kiribati waianze siku hiyo.

Takwimu za mawimbi ya bahari kituo cha Dar es salaam inaonesha kuwa wimbi kubwa zaidi ni 3.40m muda wa 1711hrs siku ya tarehe 26 lililofuatiwa na wimbi la maji kupwa la 0.35m muda wa 2324hrs.Tofauti baina yao ni (3.40-0.35)m ambayo ni 3.05m.Hili lilikuwa ni wkmb ambalo lilianza na watu wa maeneo ya Kiribati jana yake.

Alfajiri ya tarehe 27Julai kulikuwa na wimbi la ukubwa wa 3.16m muda wa 0538hrs,ikafuatiwa na wimbi la maji kupwa la 0.59m muda wa 1130hrs.Saa 1742 kulikuwa na wimbi la 3.36m na kufuatiwa na wimbi la maji kupwa la 0.35 muda wa 2352hrs.

Wimbi la 3.16m ni wkmm wakati lile la 3.36m ni wkmb lililoanza kupungua ukubwa wake baada ya siku moja tangu mwezi ulipoanza safari yake mpya.

Kumbukumbu za kuonekana mwezi kutoka moonsighting zinaonesha kuwa Dr. Youssef Ismail (MCW member), Windy Hill, San Francisco, California aliweza kuuona mwezi siku ya tarehe 25Julai.Hii ina maana siku kwao ingeanza tarehe 26Julai nyakati za Alfajiri.

Kwa upande wake Hamza Rijaal, (MCW member) wa Zanzibar aliweza kuuona mwezi kirahisi siku ya tarehe 26 nyakati za jioni.Kwa hali hiyo siku ingetofautiana kwa masaa takriban 12 na muda halisi wa kuanzwa kwa siku hiyo.

Maeneo mengine yaliyouona mwezi siku hiyo ni pamoja na Afrika kusini (SA),Malawi,Kuwait,Pakistan na kadhalika.

.....
Nms E,day next fajr.highest tide and range within 24hrs since new journey.

MWEZI SHAABAN 1427H:

Mwezi ulianza safari yake mpya muda wa 2210hrs sawa na saa 4:10 usiku tarehe 23 Agosti mwaka 2006 kituo cha Dar es salaam.

Upande wa dunia ambao kwao ni magharibi wakati huo (NMS) ni magharibi (-) ya Dar es Salaam.Kwa vile smt ni saa 12.30 magharibi hivyo kutakuwa na tofauti ya masaa 3 na dakika 40 sawa na dakika 220.

Dakika 220 ni sawa na nyuzi za longitudo $220/4=55$ (55^0 long).Ukirudi nyuzi za longitude 55 magharibi ya Dar-es –Salaam ambayo iko 39^0 E unafika 16^0 W.

Kwenye ramani mstari huo wa longitude kwa maeneo ya ikweta unaangukia kwenye bahari ya Pacific.Kwa kaskazini kidogo unapitia kwenye maeneo ya nchi kadhaa za Afrika Magharibi,ambayo ni Nouakchott-Mauritania,Morocco,Senegal,Gambia na Guinea.

Nchi hizo za Afrika Magharibi ndio wenyeji wa mwezi Shaaban 1427H. Siku ingeanza wakati inapoingia alfajiri kwao ambayo ni tarehe 24 Agosti 2006 na kudumu mpaka alfajiri ya Agosti 25.

Kwa vile hapo ni mpakani mwa siku,hivyo kila ambaye angepata muda kutekeleza ibada kama ya funga kwa kupata muda kula daku kwa vigezo vyake,basi angeipata siku hiyo.Kinyume ya hapo watasubiri hadi ifike alfajiri nyengine kwao.Ikiwa hivyo itafanya wawe wa mwisho kuipata siku hiyo na kuwa waadishaji wa siku badala ya wenyeji..

Kwa kufuatilia hali za mawimbi ya bahari tunajuwa kuwa wkmb linafanyika kwa maeneo wenyeji wa siku,huku wkmm likifanyika upande ulio kinyume na hapo.Kwa mwezi Shaaban wkmm lilifanyika 164^0 E.

Ratiba za mawimbi kituo cha Dar es salaam zinaonesha kuwa tarehe 24 alfajiri kulikuwa na wimbi la ukubwa wa 3.24m muda wa saa 11 kasoro dakika 12 alfajiri (0448).Wimbi kuu mburuziko wkmb lilikuwa la ukubwa wa 3.44m muda wa 1650 na kufuatiwa na wimbi la maji kupwa la 0.27m muda wa 2259.Hili wkmb ni wastani ya lile lililoanzwa na wenyeji wa mwezi Shaaban.Tofauti ya 3.44m na 0.27m ni 3.17m .

Tarehe 25 alfajiri kulikuwa na wimbi la 3.35m muda wa 0513hr lililofuatiwa na wimbi la maji kupwa la 0.46m muda wa 1109hr.Jioni kulikuwa na wimbi la 3.43m muda wa 1717hr kufuatiwa na wimbi la maji kupwa la 0.25m muda wa 2323hr.Tofauti yao ni 3.43m-0.25m ambayo ni 3.18m.

Kwa mujibu wa mtandao wa moonsighting ([Mwezi Shaaban 1427-H](#)), maeneo ambayo mwezi ulionekana tarehe 25 August 2006 ni pamoja na Pakistan,Kuwait na majimbo kadhaa ya Marekani.Hakuna ripoti ya Zanzibar kwa mwezi huu.Hii ina maana kuwa

mwezi mosi Shaaban kwa nchi hizo ingekuwa ni August 26.Itakuwa ni siku moja mbele na si sahihi kulingana na kalenda tunayotengeneza;ya mawimbi ya bahari.

MWEZI WA RAMADHANI 1427H

Mwezi ulianza safari yake saa tisa kasorobo mchana (1445hrs) tarehe 22 Septemba 2006 kuzingatia kituo cha Dar es salaam.

Upande wa dunia ambao ni magharibi kwao (nms) ni mashariki ya Dar es salaam.Kwa vile SMT ni saa 12.30 magharibi hivyo tofauti ya muda itakuwa ni masaa manne kasorobo (masaa3.45)=(masaa12.30-masaa8.45).

Masaa 3.45 ni sawa na dakika 225.Hizi ni sawa na kukatiza mistari ya longitude wastani wa 57.

$$225\text{min} \div 4 = 56.25^0 \text{ long.}$$

Kutokea Dar es salaam 39^0long tunakwenda mashariki 57^0long na tunafika 96^0 long

$39^0\text{long} + 57^0\text{long} = 96^0\text{long}$.Kwenye ramani mstari huu wa longitude kwa usawa wa ikweta unaangukiwa magharibi kidogo ya Indonesia.Kwa kaskazini unapita nchi ya Bangladesh (Myanmar) na China.

Hivyo wenyeji wa mwezi wa Ramadhani mwaka 1427H ni nchi za Indonesia,Bangladesh,China na maeneo yaliyo karibu nao.Siku ingeanza itakapoingia alfajiri kwa watu hao kiasi kwamba kwa kufuata ibada ya funga kila ambaye atakuwa na muda wa kuweza kula daku atakuwa ameipata siku hiyo na wengine isiyowezekana wangesubiri alfajiri inayofuata.Badala kuwa wenyeji wa siku wangukuwa waadishaji wa siku,kwa maana kuwa wangukuwa wa mwisho kujumuishwa na wote wengine ambao wako magharibi ya 96^0 long .

Kutokana na teknolojia ya mawasiliano kwa sasa inawezekana kwa watu wengine kupata taarifa ya kuanza siku kwa watu wa Indonesia na China lakini kila mmoja ambaye asingeweza kutekeleza ibada ya funga kama kigezo atahesabika kuwa yuko nyuma ya maeneo hayo.

Afajiri itakapoingia Indonesia kwa kalenda ya kikristo itakuwa ni tarehe 23 Septemba.Siku ingedumu kwa muda wa masaa 24 mpaka alfajiri ya tarehe 24 Septemba.Hivyo mwezi Ramadhani 1427H kwa kalenda ya Kikristo ilikuwa tarehe 23 na 24 Septemba 2006.

Makisio ya mawimbi ya bahari ni kwamba wkmb litafanyika maeneo ya nchi zilizo wenyeji wa mwezi.Wkmm litafanyika 180^0long kinyume na ukanda wa wenyeji.Maeneo hayo ni $96^0\text{long} + 180^0\text{long} = 276$

$$360^0\text{long} - 276 = 84^0\text{long}$$

Mstari huo(84^0) wa longitude unapitia katikati ya nchi za Canada na Amerika na upande wa magharibi wa bara la Amerika ya kusini.Hivyo wakati wa alfajiri wenyeji wa siku watakutana na wimbi hili wkmm.Kwa upande mwengine wakati siku imeanza watu wa Amerika watapata ishara ya kuanza siku alfajiri yao itakapoingia kwa kupata wkmb wakati wa magharibi ambalo ndilo lile lilionzwa na wenyeji..

Ratiba za mawimbi kituo cha Dar es salaam zinaonesha tarehe 23 alfajiri muda wa 0441hrs kulikuwa na wimbi la ukubwa wa 3.50m.Likafuatia wimbi la 0.38m muda wa 1042hrs.Tofauti baina yao $3.50\text{m} - 0.38\text{m} = 3.12\text{m}$. Muda wa 1648hrs jioni kulikuwa na wimbi la 3.44 m na kufuatiwa na wimbi la 0.27m muda wa 2250hrs.Tofauti baina yao ni

3.17m. Tarehe 24 alfajiri muda wa 0503hrs kulikuwa na wimbi la 3.56m na kufutiwa na 0.38m muda wa 1107hrs. Tofauti baina yao ni 3.18m.

Hivyo mwezi mosi Ramadhani 1427H kituo cha Dar es Salaam ilikuwa tarehe 23 Septemba 2006. Kulingana na mtandao wa moonsighting (<http://www.moonsighting.com/1427rmd.html>) maeneo ambayo yaliuona mwezi tarehe 23 septemba na hivyo Ramadhani kuanza siku hiyo ni pamoja na Colombo nchini Srilanka ambao baada ya kuuona mwezi walitangaza kuanza kwa Ramadhani usiku huo. Maeneo mengine ni Port Louis (Mauritius), Pemba (Zanzibar), South Africa, Namibia, Abuja (Nigeria), Guyana na Arizona (Amerika).

Ripoti ya Hamza Rijali wa Zanzibar juu ya kuonekana mwezi tarehe 23 Septemba ina maana mwezi mosi ulianza tarehe hiyo lakini funga yenyewe ilinza tarehe 24 Septemba. Hivyo imepatana na kalenda ya mawimbi kwa tarehe lakini imetofautiana juu ya muda halisi wa kuanza kwa ibada hiyo. Hii ndiyo hali katika tarehe zote nyengine baina ya kalenda hizi.

Kulingana na ripoti za moonsighting nchi za Bangladesh, Australia, India, Iran na Pakistan waliuona mwezi tarehe 24 na kuanza kufunga tarehe 25. Kwa kalenda yetu ya mawimbi haiwezekani kuwa watu wa kuanza Ramadhani tarehe 25. Hivyo nchi hizo zilikuwa zimetoka nje ya kalenda kuanza mwezi wa Ramadhani.

MWEZI WA SHAWWAL 1427H

Mwezi ulianza safari yake mpya muda wa 0813hrs (saa 2:13 asubuhi) tarehe 22 oktoba 2006 kuzingatia kituo cha Dar es Salaam.

Upande wa dunia ambao ni magharibi kwao muda huo ni mashariki ya Dar es Salaam. Tofauti ya muda kwa kutoka smt ni $12:30 - 02:13 =$ masaa 10:17.

Taofauti hii masaa 10.17 ni sawa na dakika $10 \times 60 + 17 =$ dakika 617.

Dakika hizi ni sawa na nyuzi za longitude $617 \div 4 = 154.25$
 $= 155^0 \text{long.}$

Kutokea kituo cha Dar es Salaam 39^0long tutakwenda 155^0 ili kuwafikia wenyeji wa mwezi Shawwal. Ni kama kwamba tutakwenda $194^0 \text{E} = 39^0 + 155^0$. Itatufikisha 166^0W . Kwenye ramani mstari huu unapita katikati ya bahari ya Pacific kusikokaliwa na watu kwa pande zote karibu na ikweta. Eneo pekee unapopitia linalokaliwa na watu ni magharibi ya jimbo la Alaska la Marekani, kaskazini ya Ikweta.

Jirani na mstari huo wa longitude karibu na ikweta ni nchi za visiwa za Kiribati na Samoa. Miji mikubwa inayokaliwa na watu ni Bariki, Funafuti na Apia. Hivyo wenyeji wa mwezi wa Shawwal ni visiwa vya Kiribati na Samoa. Wengine ni Amerika.

Bila kuzingatia mapitio ya International Date Line ambao upo maeneo hayo, ni kwamba siku ya kiislamu itanza itakapoingia alfajiri kwa wakaazi wa Kiribati na Samoa. Itakuwa ni tarehe 23 oktoba na kudumu mpaka alfajiri ya tarehe 24 oktoba 2006. Mwezi huu na uenyeji wa nchi hizi ni mfano halisi wa namna kalenda ya kiislamu ya mawimbi ya bahari inavyotafautiana na kalenda ya inayotumika sasa na hata waislamu..

Kwa teknolojia ya mawasiliano iliyopo hata iwapo itapatikana taarifa ya kuonekana mwezi popote pale basi haipasi kuanza siku kabla ya nchi wenyeji wa mwezi Shawwal tuliowataja hapo juu kuanza na wao kuwa viongozi wa siku hiyo.

Makisio ya mawimbi ya bahari ni kuwa wkmb litafanyika eneo la wenyeji nyakati za jioni/magharibi. Wimbi la wkmm litafanyika upande ulio kinyume na hapo wakati wa alfajiri kwa nchi wenyeji. Kama tulivyoona kabla kwamba wimbi lolote kati ya wkmb na

wkmm hubaki eneo lake na kusogea kidogo tu kwa masaa 24. Hivyo kila nchi lazima itakutana na moja wapo kati ya mawimbi hayo nyakati za alfajiri na magharibi.

Ratiba za mawimbi kituo cha Dar es salaam zinaonesha kuwa tarehe 23 ambayo itakuwa ndio mwezi mosi Shawwal kulikuwa na wimbi la 3.60m muda wa alfajiri 0432hrs. Ikafuatiwa na wimbi la maji kupwa la 0.39m muda wa 1041hrs. Tofauti ya mawimbi haya ni 3.21m na hii ndio kubwa zaidi kwa Shawwal.

Kumbukumbu za kuonekana mwezi wa Shawwal mwaka 1427H kwa mtandao wa moonsighting (<http://www.moonsighting.com/1427shw.html>) zinaonesha kuwa sherehe za Iddi mwaka huo zilikuwa ni miongoni mwa mikanganyiko mikubwa ya kalenda ya kiislamu. Wako waliosherehekea tarehe 22. Wengine tarehe 23. Hawa makundi mawili wanapingwa vikali na wahusika wa mtandao huu. Wako waliosherehekea Sikukuu tarehe 24 kwa kuuona tarehe 23, wengine tarehe 24 na wengine tarehe 25.

Tanzania, kulingana kwa mwezi huo wa Shawwal ndio waliokuwa kioja zaidi, kwani walisherehekea tarehe zote nne kuanzia tarehe 22.

Matokeo hayo ni kinyume na kalenda yetu ya mawimbi ya bahari ambapo mwezi mosi Shawwal ulikuwa unaangukia tarehe mbili tu za kalenda ya kikristo nazo ni 23 na 24. Kwa Tanzania tarehe halisi ilikuwa ni 23 oktoba.

MWEZI DHUL QA'ADA 1427H

Mwezi ulianza safari yake saa saba na dakika kumi na saba (7.17) usiku wa manane (0117hrs) tarehe 21 Novemba 2006 kuzingatia kituo cha Dar es salaam.

Upande wa dunia ambao ni magharibi kwao (Nms) ni magharibi ya Dar es salaam. Tofauti ya muda kutoka SMT ni:

$$\begin{array}{r} 7:17 \\ - 0:30 \\ \hline \text{masaa 6 : dakika 47} \end{array}$$

Masaa 6 dakika 47 sawa na dakika $(60 \times 6) + 47 = 360 + 47$

$$= 407$$

Dakika 407 ni sawa na nyuzi za longitude $407 \div 4$

$$= 102^0 \text{ long.}$$

Kwenye tufe la ramani ya dunia ukirudi nyuzi 102 magharibi ya Dar es salaam ili kufika Greenwich ni $(102 - 39)^0 \text{ long} = 63^0 \text{ long W.}$

Mstari huu wa longitude unapita katikati ya bara la Amerika ya kusini kwenye nchi za Brazil, Bolivia, Venezuela na Argentina. Kwa kaskazini unapita mashariki ya Canada. Hivyo wenyeji wa mwezi Dhulqa'da mwaka 1427H itakuwa ni nchi hizo na zile zilizo karibu nao kama vile Colombia. Siku itaanza itakapoingia alfajiri kwao na yeyote mwengine hata akipata taarifa ya kuonekana mwezi hapaswi kuwatangulia wenyeji hawa katika kuianza siku na mwezi.

Kwa wale walio jirani mashariki na magharibi ya long. ya 63 wataanza siku pamoja nao pindi wakiwa na muda wa kutekeleza ibada ya funga kama kigezo kwa kuwa katika uwezekano wa kula daku. Isipowezekana hivyo watakuwa waadishaji wa siku badala ya kuwa wenyeji.

Makisio ya mawimbi ya bahari ni kwamba kutakuwa na wimbi kuu mburuziko la kufikirika eneo walipo wenyeji. Wimbi mmiminiko (wkmm) litatokea upande wa pili ulio kinyume na wao kwenye mviringo wa dunia, takriban nyuzi 180 kuelekea upande wowote kutoka long 63^0W

$$63^{\circ} \text{ W} + 117^{\circ} \text{ E} = 180^{\circ}$$

$$(180^{\circ} - 63^{\circ}) \text{ W} + (180^{\circ} - 117^{\circ}) = 180^{\circ}$$

Eneo hilo itakuwa ni Long 117° E ambazo ni Indonesia kwenye ikweta, China kwa kaskazini na Australia kwa kusini.

Tanzania na nchi za Afrika kwa mwezi huu ilikuwa wako nyuma ya siku ingawa nchi wenyeji akina Brazil wako nyuma ya Tanzania katika mzunguko wa Dunia. Tanzania ingekutana na Wkmm ambalo liko Indonesia mapema kuliko Brazil tarehe 21 Novemba lakini siku ingeanza alfajiri ya tarehe 22 Novemba baada ya kutangulia wenyeji. Kwa kuzingatia wenyeji siku ingedumu mpaka alfajiri ya tarehe 23 Novemba. Wkmb kwa mwezi huu kulingana na kituo cha Dar es salaam lingechelewa kukutana nalo.

Tangu uchambuzi wa mawimbi miezi iliyotangulio tunapofika hapa ndio huwa tunafungua kitabu cha ratiba za mawimbi ya bahari kwa mwaka 2006. Kwenye ratiba hiyo inaonesha kuwa tarehe 21 Novemba alfajiri muda wa 0405hrs kulikuwa na wimbi la ukubwa wa 3.55m.

Tarehe 22 Novemba alfajiri muda wa 0436hrs kulikuwa na wimbi la ukubwa wa 3.59m ambalo ndilo kubwa zaidi kwa mwezi huo lililofuatiwa na wimbi la maji kupwa la 0.46m muda wa 1055hrs ambalo ndilo dogo zaidi kwa mwezi huo. Tofauti baina yao ni 3.59m - 0.46m = 3.13m ambayo ndiyo kubwa zaidi. Mawimbi mengine ni kamba ilivyo katika kalenda ya mfano ya 1427H ambayo imeambatishwa na makala hii.

Kuanzia sasa kila mara katika kutengeneza kalenda ya mfano huwa ndio tunaangalia matokeo ya kumbukumbu za uonekanaji mwezi kwa mwaka 2006. Kume kuwa na kukubaliana kati ya Nms na sehemu ambazo zinatajwa na mtandao wa moonsighting kwamba mwezi utaonekana kwa macho bila msaada wa vifaa vya kuonea.

Katika kumbukumbu hizo za moonsighting.com mwezi wa Dhul qa'ada 1427H (<http://www.moonsighting.com/1427zqd.html>) inaonesha kuwa waliouna mwezi tarehe 21 na hivyo kuanza siku tarehe 22 ni Afrika kusini (South Africa) katika miji ya Durban na Cape town pamoja na miji ya America. Hata hivyo nchi nyingi ziliuona mwezi tarehe 22 Novemba na kuanza siku tarehe 23. Hii ingepelekea siku hiyo kutoka nje ya kalenda yetu kwa masaa kadhaa.

MWEZI DHUL HIJAH 1427 H

Ulianza safari yake tarehe 20 Disemba muda wa saa 11 jioni (1700hrs) kwa kuzingatia kituo cha Dar es salaam.

Nms ni mashariki ya Dar es salaam. Tofauti kutoka SMT itakuwa ni masaa 1.30
(12.30-11.00) = saa 1.30

Muda wa saa 1.30 ni sawa na dakika 90 ambazo ni sawa na nyuzi za longitude $90 \div 4 = 22.5$ wastani wa 23° long.

Kwenye ramani 23° long E ya Dar es salaam (39° long) inatupeleka mpaka ($39 + 23$)⁰ long 62° long E. Hapo ni katikati ya bahari ya hindi maeneo yasiyokaliwa na watu kwa usawa wa ikweta. Upande wa kaskazini unapitia nchi za Pakistan, Iran, Kazakhstan na sehemu ya Urusi..

Wenyeji wa mwezi Dhulhijja itakuwa ni nchi hizo hapo juu na nchi zilizo jirani nao. Siku itaanza kwao itakapoingia alfajiri tarehe 21 Disemba. Watu wengine wote hawatoweza kuanza siku na mwezi huu hata kama taarifa zitawafikia isipokuwa kama wataweza kuchangia alfajiri kuwezesha kufanya ibada ya funga kwa vigezo vya muda wa kula

daku.Kudumu kwa siku hiyo ya kiislamu ni mpaka alfajiri inayofuata ambayo kwa kigezo cha wenyeji ingekuwa ni tarehe 22 Disemba 2006.

Makisio ya mawimbi ya bahari ni kupatikana wkmb eneo la wenyeji na wkmm upande wa pili wa dunia nyuzi 180° upande wowote kutoka walipo wenyeji.

Kwa kuelekea mashariki kwanza ni $(180 - 62)^{\circ}E = 118^{\circ}$.Tunahitaji 62° kukamilisha mzunguko kutufikisha eneo la wkmm ambazo tutazitoa kutoka $(180-62)^{\circ}W = 118^{\circ}W$.Kwenye ramani mstari huo kwa kaskazini ya ikweta unapita magharibi ya Canada na Marekani.Sehemu nyengine unaangukia maeneo ya bahari ya Pacific yasiyokaliwa na watu.

Siku kwa kituo cha Dar es salaam kama kiwakilishi haikupitana sana katika kuanza kwake.hivyo kwa tarehe ya kalenda ya kikristo ilikuwa ni tarehe ile ile ya wenyeji;21 Disemba.

Ratiba ya mawimbi ya bahari inaonesha kuwa tarehe 21 kulikuwa na wimbi la ukubwa wa 3.56m alfajiri ya 0425hrs,likafuatia wimbi la maji kupwa la 0.42m muda wa asubuhi 1048hrs.Jioni muda wa 1656hrs kulikuwa na wimbi la maji kujaa la 3.05m kufuatiwa na wimbi la maji kupwa la 0.69m muda wa usiku wa 2243hrs.Ilipofika alfajiri tena muda wa 0502hrs kulikuwa na wimbli la 3.61m ikifuatiwa na 0.38m muda wa 1121hrs.Wimbi la 3.56m ni mwendelezo wa wkmm,wakati lile la 3.05m likiwa ni mwanzo wa wkmb.

Wimbi kubwa zaidi ni 3.61m lililofuatiwa na dogo zaidi kwa mwezi huo,la 0.38m.Tofauti baina yao ni $3.61m - 0.38m$ ambayo ni 3.23m na ambayo ndiyo kubwa zaidi kwa mwezi Dhulhijja.

Kumbukumbu za kuonekana mwezi na tarehe za Idul Hajj kwa mwaka huo za moonsighting.com (<http://www.moonsighting.com/1427zhj.html>) zinaonesha kuwa nchi na maeneo yaliyoweza kuuona mwezi tarehe 21 Disemba 2006 ni pamoja na mji wa Esfahan (Iran),Kuwait,Mauritius,Algeria na miji mbali mbali ya United States of America.

Kwa mujibu wa kumbukumbu hizi sikukuu rasmi ya Idul Hajj kwa Tanzania ilikuwa ni Jumapili tarehe 31 Disemba 2006.Ina maana mwezi mosi Dhulhijja ilikuwa ni tarehe 22 Disemba.Mara nyingi siku rasmi inayofahamika nje ya Tanzania huwa ni ile inayofuatwa na Serikali na Bakwata.Mara nyingi Bakwata huwa wanachelewa kwa siku moja ukilinganisha na wenzao Ansaar Sunnah.Hivyo kwa Tanzania wako walioanza tarehe 21 na hivyo Idul Hajj kuwa ni Jumamosi tarehe 30 Disemba.

Katika mchoro wa kuonekana mwezi kwenye mtandao wa moonsighting kuna rangi nne zinazotumika kueleza kuoneka huko kwa mwezi:

A-kijani, kwa ajili ya sehemu unapoonekana kwa macho ya kawaida na kwa urahisi.

B-Blue, kwa ajili ya kuonekana iwapo tu hali ya hewa ni nzuri kwa mwangaliaji.

C-Kijivu,kwa ajili ya mwangaliaji anayetumia darubini tu kuungalia mwezi.

D-Nyekundu,kwa eneo ambalo hakuna uwezekano kuonekana mwezi.

Jambo la kumshukuru Allah(S.W) ni kuwa ncha ya mashariki ya eneo A (la kijani) linakubaliana na eneo ambalo katika mjadala huu tumeliita la wenyeji wa mwezi.Hii ina maana mjadala huu umekubaliana na matumizi ya vifaa vya kiteknolojia ya anga.

